

HakiRasilimali
Transparency & Accountability
for the Extractive Industry

PUBLISH WHAT YOU PAY

# SERA YA JINSIA YA MGODI WA NTABALALE

## Kuimarisha Usawa wa Kijinsia katika Sekta ya Uchimbaji Mdogo

DISEMBA 2024

# Yaliyomo


1. Tafsiri
2. Utangulizi
3. Dhana ya Sera
4. Upeo wa Sera
5. Kanuni Tangulizi
6. Malengo ya Sera
7. Sehemu za Sera
    - 7.1 Kutengeneza Mazingira Wezeshi
    - 7.2 Ajira za Wafanyakazi
    - 7.3 Mazingira ya Kufanya Kazi
    - 7.4 Usalama na Afya Mahala pa Kazi
    - 7.5 Unyanyasaji wa Kijinsia
    - 7.6 Unyanyasaji na Ubaguzi
    - 7.7 Likizo ya Uzazi na Malezi

# 1. TAFSIRI

**Jinsia** ni dhana inayohusiana na tabia na majukumu yanayotokana na tamaduni na jamii, na siyo tu tofauti za kimaumbile za kiume na kike.

**Uchimbaji Mdogo wa Madini** ni mfumo wa uchimbaji wa madini usiorasmi unaomilikiwa na kusimamiwa na Wizara ya Madini.

**Mgodi wa Ntabalale** ni mgodi wa uchimbaji mdogo wa dhahabu ulioanzishwa mwezi Juni, 2019, na unamilikiwa rasmi kwa leseni namba PML 0164KHM chini ya Wizara ya Madini. Mgodi huu upo mkoani Shinyanga, wilayani Kahama, na unawaajiri wafanyakazi wa jinsia zote, yaani wanaume na wanawake. Mgodi umejikita katika kuhakikisha usimamizi wa haki za kibinadamu, ikiwa ni pamoja na usawa wa kijinsia.

**Ukatili wa Kijinsia,** ni aina yoyote ya ukatili au madhara yanayofanywa dhidi ya mtu kwa sababu ya jinsia yake. Mara nyingi, ukatili hutokana na tofauti za kijinsia, ubaguzi, au mifumo ya nguvu isiyo sawa kati ya wanaume na wanawake. Ukatili wa kijinsia unaweza kuathiri watu wa jinsia zote, lakini wanawake, wasichana, na watu wamakundi yanayonyanyapaliwa mara nyingi huwa wahanga wakubwa.

**Usawa wa Kijinsia,** ni hali ya kuhakikisha kuwa makundi yote kwenye jamii wanapata haki, fursa na rasilimali kwa usawa bila kujali jinsia yao

**Ubaguzi wa Kijinsia** inatafsiriwa kama ubaguzi kulingana na jinsia ya mtu inayolenga kumuathiri utambulisho wake na kunyima uhuru katika siasa, Uchumi, kijamii na kiutamaduni.

**Unyanyasaji wa Kijinsia,** ni aina yoyote ya tabia au kitendo kinachomlenga mtu kwa misingi ya jinsia yake na kinacholenga kumdhalilisha, kumtweza au kumweka katika hali ya kutostarehe, hofu, au hatari. Unyayasaji huu unaweza kutokea katika mazingira ya nyumbani, kazini, shuleni, au sehemu nyingine za kijamii na mara nyingine hutokana na tofauti za nguvu au mamlaka kati ya watu na jinsia tofauti.

**Unyanyasaji wa kijinsia** unaweza kuchukua sura mbalimbali zikiwamo (lakini hata zaidi ya ): Maneno yenye mwelekeo wa kingono, kama vile maoni kuhusu maumbile ya mwajiriwa, maswali kuhusu mahusiano yake ya kingono au utani unaoudhi. Ishara au vitendo kama vile kuonesha picha za kingono au picha halisi, kumchungulia mtu, kutoa ishara au maandishi yanayoashiria ngono. Vitendo kama kujigusisha, kushika au kupapasa, kushambulia (jaribio au tishio la kufanya vitendo hivyo)

# 2. UTANGULIZI

Sekta ya Uchimbaji Mdogo Tanzania ni moja ya sekta inayochangia vyema kiuchumi, kuimarisha pato la wachimbaji na Maisha yao ikiwemo wanawake wengi waliopo kwenye sekta hii. Licha ya mchango wao katika Sekta hii wanawake wengi wameendelea kupitia changamoto za ufinyu wa fursa zilizopo katika sekta ya madini na hivyo kupelekea kukosekana kwa usawa wa kushiriki katika fursa za kiuchumi.

Vikwazo vya kimfumo ikiwemo mila na desturi kandamizi zinazolenga kuzuia ushiriki ukamilifu wa wanawake katika kumiliki leseni za uchimbaji wa madini, kupata mikopo ya fedha na vifaa, taarifa ya kijielojia Pamoja na kukosekana kwa vifaa vya kisasa katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini vinamkwamisha mwanamke kukua kiuchmi katika sekta ya madini.

Mgodi wa Ntabalale, unalenga kupambana na changamoto za kijinsia kwa wanawake walio sehemu za ajira za mgodi Pamoja na wanaoshiriki katika shughuli mahala pa kazi. Lengo ikiwa ni kupunguza vikwazo vya usawa wa kijinsia na kutambua mchango wa mwanamke katika shughuli za uchimbaji.

Kulingana na mfumo wa uchimbaji mdogo kuwa na ajira ndogo ndogo kwa wingi mahala pa kazi, ni muhimu kusisitiza juu ya kuimarisha mfumo wa usawa wa kijinsia. Na kutokana na mfumo wa uchimbaji kuwa na waajiriwa wengi wa jinsia ya Me mahali pa kazi Mfano sehemu ya maduara ambapo shughuli nyingi zinafanyawa na wanaume na sio jinsia ya Ke kulingana na aina ya kazi na nguvu inayohitajika katika kufanya kazi hiyo.

Sera hii inalenga kupunguza na kuondoa kabisa ubaguzi wa kijinsia na kuchochea usawa wa kijinsia mahala pa kazi na kulenga kuwezesha wanawake kupata usawa wa fursa zilizopo katika sekta ya madini. Ikiwemo kuondosha mila na desturi kandangamizi zinazolenga kumkandamiza mwanamke mahala pa kazi.

Vilevile sera hii inalenga kuondosha ubaguzi na unyanyasi wa kijinsia wa wanawake kwa lengo la kuboresha nafasi ya mwanamke katika kushiriki shughuli za kiuchumi na kufanya maamuzi yanayohusiana na kazi au binafsi mahala pa kazi pamoja na kuheshimu mawazo yao.

# 3. MUKUTADHA WA SERA

Dhana ya sera hii ni kuhimiza usawa wa kijinsi na kuhakikisha ushiriki wa usawa wa mwanamke katika haki na fursa za kiuchumi zilizopo katika sekta ya uchimbaji mdogo.

# 4. WIGO WA SERA

Sera hii ya jinsia itatumika kwa wahusika wote wa shughuli za uchimbaji mdogo wa madini ikiwemo:

## I. Waajiri:

Ikiwepo kampuni za madini, wamiliki wa leseni za uchimbaji na wamiliki wa leseni za wafanya biashara zinazojihusisha na uchimbaji wa madini.

## II. Waajiriwa:

Wafanyakazi wote katika uchimbaji wa madini waliopo katika uchimbaji wa leseni kubwa, kati na mdogo.

## III. Wakandarasi na kandarasi ndogo:

Kampuni na watoa huduma na vifaa katika sekta ya uchimbaji madini ikiwemo ujenzi, usafirishaji, na taaluma tofauti katika uchimbaji.

## IV. Wawekezaji na Wawezeshaji:

Kwa wale wanaowezesha mitaji au huduma za kifedha katika uchimbaji wa madini kwa njia ya uwekezaji wa moja kwa moja au kupitia taasisi za kifedha.

## V. Watumishi wa Serikali na Wasimamizi:

Watumishi wa Serikali na wasimamizi wanaohusika katika kuratibu na kusimamia sekta ya madini, utekelezaji wa sheria na kanuni zake.

## VI. Watoa huduma na wauzaji:

Kampuni na wahusika wanaojihusisha katika kutoa huduma za vifaa, machine na vifaa muhimu vinavyohitajika katika usimamizi wa uchimbaji wa madini.


## VII. Wadau wa Jamii:

Wadau wa jamii hususani waliopo kwenye maeneo yanayojihusisha na shughuli za uchimbaji na madini Pamoja na wale ambao shughuli za madini zinawaathiri moja kwa moja au kwa namna moja au nyingine.

Sera hii inalenga kukidhi umuhimu wa kutambua haki za mwanamke mahala pa kazi, kuhimiza usawa wa kijinsia katika kila Nyanja ya shughuli za uchimbaji wa madini. Hasa katika kuimarisha mazingira ya ufanyaji kazi kwa wanawake na ushiriki wao katika shughuli za uchimbaji wa madini kwa lengo la kukuza kipato na kuboresha hali ya maisha kutokana na shughuli za uchimbaji.


Vilevile sera hii inatambua changamoto zilizopo katika sekta ya madini wanazokutana nazo wanawake wachimbaji ikiwemo ukosefu wa mitaji, ubaguzi na ukatili wa kijinsia, Pamoja na afya na usalama. Kupitia muongozo huu sera hii inalenga kukabili dhana hizi potofu na kutengeneza mazingira jumuishi na salama kwa wanawake wachimbaji.

# 5. KANUNI TANGULIZI



## I. Usawa

Sera hii imejengwa katika kanuni ya usawa kwa lengo la kuhimiza usawa wa kijinsia kwa kuhimiza ushiriki wa wanawake katika kutambua fursa na kuheshimiwa sawasawa na jinsia Me.



## II. Kutokuwa na Ubaguzi

Sera inalenga kukataza mifumo yeyote ya ubaguzi ikiwemo ubaguzi wa kijinsia na kuchochea desturi ya kuheshimu jinsia zote.



## III. Uwezeshaji

Sera hii inalenga kumwezesha mwanake katika upatikanaji wa rasilimali, furs ana uwezo wa kufanya maamuzi.



## IV. Ushiriki na ujumuishaji

Sera hii inalenga kupima ushiriki wa wanawake katika kuweka mipango na kufanya maamuzi.





# 6. MALENGO YA SERA

- **I.** Kuhimiza Usawa wa Kijinsia.
- **II.** Kuweka mazingira salama na wezeshi kwa jinsia zote.
- **III.** Kuweka misingi ya kufikia usawa kwa mafunzo, uendelezaji wa taaluma za ajira na fursa za ukuaji.
- **IV.** Kuzuia na kushughilikia unyanyasaji na ubaguzi.
- **V.** Kuwezesha mazingira ya usawa katika kazi na Maisha katika likizo ya uzazi na malezi.
- **VI.** Kuhimiza mafunzo ya kuongeza ufahamu wa masuala ya kijinsia hasa kwa wafanyakazi katika shughuli zao mahala pa kazi.
- **VII.** Kujenga mazingira jumuishi mahala pa kazi na kuondoa mifumo yeyote ya unyanyasi na ubaguzi.

# 7. SEHEMU ZA SERA

## 7.1. Kutengeneza mazingira wezeshi

Sera hii inalenga kuhakikisha usawa wa kijinsia na kutokuwa na ubaguzi katika maeneo yote ya mgodi. Kuhimiza ukuaji wa ushiriki wa jinsia zote za Me na Ke katika shughuli za Mgodi Pamoja na kufanya maamuzi.

- i. Kuhimiza ushiriki wa wanawake katika ngazi zote za usimamizi wa mgodi.
- ii. Kuhakikisha kuwa muda wote wanawake wanahusishwa ipasavyo na kuwakilishwa ipasavyo katika ngazi ya usimamizi ikiwemo idara ya usalama, usimamizi wa fedha, na usimamizi wa mahala pa kazi.

## 7.2. Ajira za wafanyakazi

Mgodi wa Ntababale utahakikisha ajira za wafanyakazi zinapitia mchakato utakaohusisha: -

- i. Kuhakikisha kutoa kipaumbele katika kuajiri na kuwa na idadi yakutosha ya wafanyakazi wa jinsia ya Ke ili kuhakikisha usawa katika nafasi za ajaira.
- ii. Katika hatua ya kuajiri na kukuza nafasi za ajira wanawake wapewe nafasi ya asilimia 50%
- iii. Kuhakikisha mikataba inayosimamia uhusiano wa mwajiri na mwajiriwa uwe kwenye lugha ambayo inaeleweka na pande zote mbili.
- vi. Kuhakikisha usawa wa malipo kwa jinsia zote za wafanyakazi katika maeneo yote ya mgodi.
- v. Kuhakikisha kuwa muda wa kuwepo kazini na ule wa mapumziko uheshimiwe na pande zote za mwajiri na mwajiriwa bila kuhusisha Jinsia.

vi. Kuhakikisha kuwa waajiriwa wote wanapata haki ya mapumziko ikiambatana na malipo yao bila kuhusisha jinsia zao.
vii. Kuhakikisha wafanyakazi wa mgodi wanao uwezo wa kupata likizo ya uzazi na malezi ikiambatana na malipo ikitambulishwa kwenye mikataba yao ya ajira.
viii. Kuhakikisha kuwa wafanyakazai wote wana haki zinazotambulishwa kwenye mikataba yao kipindi cha kusitisha mikataba bila kuhusisha jinsia zao.

## 7.3. Mazingira ya kufanya kazi

Mgodi wa Ntababale utahakikisha mazingira salama mahali pa kazi kwa kuzingatiayafuatayo:

i. Ukaguzi wa kila wakati katika mazingira ya mahala pa kazi ambayo yanaweza kuleta viashiria vya kutokuwa na sehemu salama kama vile kukosekana kwa mahala rasmi kwa wanawake kufanya kazi.
ii. Kupatikana kwa huduma za msalani ambazo ni safi na salama zilizotenganishwa kwa jinsia Ke na Me.
iii. Kuajiri maafisa usalama wa jinsi Ke kwa lengo la kusimamia wafanyakai wa jinsia Ke katika ukaguzi wa usalama mahala pa Kazi.

## 7.4. Usalama na Afya Mahala pa Kazi

Mgodi wa Ntababalale utahakikisha kuwa usalama na afaya vinazingatiwa wakati wote mahala pa kazi kwa kuzingatia yafuatayo:-

i. Utoaji wa vifaa kinga kwa wafanyakazi wote waliopo mahala pa kazi pasipo kuhusisha jinsia zao.
ii. Utoaji wa mafunzo kwa wafanyakazi wote juu ya afya na usalama mahala pa kazi.
iii. Utoaji wa huduma ya kwanza kwa wafanyakazi wote waliopata ajali mahala pa kazi na wale ambao wapo katika matumizi ya kemikali zenye viambata sumu.

## 7.5. Unyanyasaji wa Kijinsia

Mgodi wa Ntababale unapinga Unyanyasaji wa Kijinsia ikiwa ni hali ya mtu kujisikia kubughudhiwa kutokana na vitendo, maneno, tabia za mtu mwingine vinavyoashiria, kumtaka au kumuomba uhusiano wa kingono. Vitendo vinaweza kuelekezwa kwa mtu mmoja, kundi la watu au kwa kila mtu na inaweza kuwa ni kitendo kimoja kilichotendwa mara moja au tabia inayojirudiarudia. Madhara ya unyanyasaji wa kijinsia ni kumdhalilisha mtu mwingine, kuweka mazingira ya vitisho, uadui, kushusha hadhi, kuwaondolea utu au kuwaudhi walengwa au watu wengine.

## 7.6. Unyanyasaji na Ubaguzi

i. Muda wote Mgodi wa Ntababale utaanzisha taratibu za kutoa taarifa na kuhusiana na unyanyasi wa kijinsia na ukatili wa kijinsia.
ii. Muda wote Mgodi wa Ntabalale utaweka utaratibu wa kutoa adhabu kali kwa vitendo vinavyohusishwa na unyanyasaji na ubaguzi wa kijinsia.

## 7.7. Likizo ya Uzazi na Malezi

i. Mgodi wa Ntabalale utahakikisha likizo ya uzazi na malezi ikiambatana na malipo kamili kulingana na mkataba wa ajira ya mfanyakazi.
ii. Mgodi wa Ntabalale unaendelea kuhimiza jinsia zote kuendelea kushirikiana katika majukumu ya shughuli za mahala pa kazi pamoja na nyumbani.

P. O. Box 38486
Dar es Salaam, Tanzania
+255 (0) 745 655 655
info@hakirasilimali.or.tz
www.hakirasilimali.or.tz